MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

WFT

MAPENDEKEZO YA MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA TANZANIA

KUHUSU JINSI YA KUINGIZA MASUALA YA USAWA WA JINSIA KATIKA RASIMU YA PILI YA KATIBA YA TANZANIA

KWA NINI MISINGI YA USAWA WA JINSIA ILINDWE KATIKA KATIBA MPYA?

Madhumuni ya Jedwali

Madhumuni ya Jedwali hili ni kuwawezesha Wabunge (wanawake kwa wanaume) katika Bunge Maalum la Katiba, na wanaharakati wa jinsia na haki za wanawake kuimarisha hoja zao kuhusu utetezi wa kulinda misingi ya usawa katika Katiba Mpya.

Tujikumbushe Dhana ya Usawa wa jJnsia Ni Nini?

Usawa wa jinsia ni hali ya wanawake na wanaume kuwa na fursa sawa na upatikanaji wa haki zenye kuleta tija, katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya jamii, kati ya makundi haya mawili. Lengo kuu la kuwepo kwa usawa wa jinsia likiwa ni kuhakikisha raia wote wanapewa nafasi ya kukua na kuondolewa vikwazo mbalimbali ili waweze kuchangia na kutambuliwa kwa usawa katika maendeleo yao ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa.

Katiba Yenye Mrengo wa Jinsia ('Gender Sensitive Constitution) Inafananaje?

Hii ni Katiba:

i). Iliyotokana na mchakato uliyoshirikisha sauti za wanawake na wanaume wakati wa uandaaji wake, na iliyoweka bayana makubaliano ya misingi mikuu itakayoongoza nchi yetu ikibeba sauti hizo.

ii). Inayozingatia misingi ya demokrasia, ikiwepo utawala wa sheria na unaowajibika kwa wananchi, usawa wa jinsia, na utu na heshima yaa kibinadamu kwa kila raia- wakiwemo wanawake na wanaume, watoto wa kike na wa kuime.

ii). Aidha inayowezesha kuwepo kwa misingi mikuu ya usawa kati ya wanaume na wanawake katika vipengele mbalimbali vya Katiba.

Kwa Nini Misingi Ya Usawa Wa Jinsia Iwepo Katika Katiba Mpya?

Katiba ni **SHERIA MAMA** inayolinda haki za raia wote (wanawake, wanaume na watoto) nchini, na kuainisha mfumo wa kuendesha nchi na wajibu wa viongozi wanaopewa dhamana ya kuongoza. Hivyo ni muhimu SHERIA HII MAMA iwe imebeba masuala/haki za makundi haya mbalimbali nchini kwa kudumisha maendeleo yenye tija.

Hoja Za Wanawake Zinasimamia Wapi?

Usawa wa jinsia ni msingi muhimu kwenye maendeleo ya nchi yeyote ikiwemo nchi yetu ya Tanzania. Tafiti mbalimbali nchini na kwingineko zimeonyesha kuwa kwenye sekta ambazo zina tekeleza mipango yenye kulenga katika kukidhi mahitaji ya wanawake na wanaume, na, kutambua michango yao mbalimbali zimeleta zaidi tija kimaendeleo kuliko sekta ambazo kawaida hazilengi katika kuleta usawa wa jinsia kwenye ngazi mbalimbali za utekelezaji. Pia, ujenzi wa misingi ya usawa wa jinsia kwenye Katiba mpya ni muhimu kwa kuwa Tanzania ni nchi mojawapo ya Afrika/Ulimwengu ambayo imesaini Mikataba mingi ya kimataifa na kikanda ya kutekeleza katiba, sera, sheria na mipango iliyojengewa kwenye misingi ya usawa wa jinsia nchini. Mikataba hii inajumuisha: Mkataba wa Kimatifa wa Kuondoa Aina Zote Za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW); na Mkataba wa Kimatifa Wa Haki Za Watoto, Mpango Wa Utekelezaji Wa Mikakati Ya Bejing, Protokali Ya Makubaliano Ya Haki Za Binandamu Na Usawa Wa Jinsia Ya Umoja Wa Afrika–na mIngine mingi.

Tujikimbushe Madai Ya Haki Za Wanawake Katika Katiba Mpya:

1. Haki za Wanawake zibainishwe kwenye Katiba Mpya.
2. Sheria Kandamizi zibatilishwe.
3. Haki ya kufikia, kutumia, kunufaika na kumiliki rasilimali ya nchi.
4. Utu wa mwanamke ulindwe.
5. Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Wanawake.
6. Haki sawa katika nafasi za uongozi.
7. Haki za Wanawake wenye Ulemavu.
8. Haki ya Uzazi Salama.
9. Haki za Watoto wa Kike.
10. Haki ya kufikia na kufaidi huduma za msing.
11. Wajibu wa Wazazi katika Matunzo ya Watoto.
12. Katiba iunde chombo maalum kitakachosimamia haki za wanawake katika maeneo yote ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Tutafanikisha Uwepo Wa Katiba Yenye Mrengo Wa Jinsia Kwa Njia Mbili:

i). Kuingiza haki mahsusi ('gender specific') za wanawake na watoto wa kike katika Katiba.

ii). Kuingiza misingi imara ya usawa wa jinsia na ile inayolinda haki za wanawake ('gender equality outcomes') katika vipengele mbalimbali vya Katiba.

Jedwali hili linatoa mifano halisi ya jinsi ya kuingiza masuala ya haki za usawa wa jinsia katika vipengele mbalimbali vya Rasimu ya Pili ya Katiba au Katiba Mpya.

MAPENDEKEZO YA MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA TANZANIA KUHUSU JINSI YA KUINGIZA MASUALA YA USAWA WA JINSIA KATIKA RASIMU YA PILI YA KATIBA YA TANZANIA

JEDWALI HILI LIMEANDALIWA NA MASHIRIKA WASHIRIKI WA MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA TANZANIA[1]

IBARA INAVYOSOMEKA	UPUNGUFU/ PENGO	MAPENDEKEZO
UTANGULIZI: Kwa kuwa sisi wananchi wa Jamhuri….. Utangulizi uk.1, Para 2	Katika ufafanuzi wa dhana mbalimbali kwenye Utangulizi, dhana ya "binadamu, wananchi, raia, watu", hazikufafanuliwa. Dhana hizi mara nyingi hutoa sura ya wanaume zaidi	**Pendekezo:** Dhana hizi zinyambuliwe na kufafanuliwa kuonyesha kuwa zinawalenga wanawake na wanaume – wakiwa wote wananchi wa Tanzania • Hivyo ibara ya1ya Utangulizi isomeke: Kwa kuwa sisi wananchi, wanaume na wanawake wa Jamhuri…. **Hoja:** • Kwa kuwa mchakato huu umetokana na ridhaa ya wananchi, wanawake kwa wanaume ni vizuri kubainisha matumizi ya dhana zinazotumika kwenye

[1]Mtandao wa Wanawake na Katiba unaratibiwa na shirika la Women Fund Tanzania (WFT) na unahusisha mashirika yanayotetea haki za Wanawake na Binadamu yakiwemo yafuatayo: Equality for Growth (EFG), Haki za Wanawake (HAWA), Kilimanjaro Women Information Exchange Consultancy Organisation (KWIECO), Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA), Shirikisho la Vyama vya Walemavu (SHIVYAWATA),Tanzania Media Women Association (TAMWA), Tanzania Gender Networking Programme (TGNP) , Tanzania Women Cross Party (TWCP-ULINGO) , Trade Union Congress of Tanzania (TUCTA) , Tumaini Women Development Association (TUWODEA) , Women Fund Tanzania (WTF) , Women Legal Aid Centre (WLAC) , Zanzibar Gender Coalition (ZGC) , KIVULINI , Wote Sawa , Jitolee kishapu , ADC Foundation , Saida Wazee Tanzania (SAWATA) , Women in Law and Develepment in Africa (WILDAF) , Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA) , Tanzania Women Miners Association (TAWOMA), Jukwaa la Katiba na Wanawake wanaharati binafsi , KBH Sisters , Warembo Forum, Binti Leo CulturalWpmen Group, SWAUTA , Childrens dignity forum ,CCRBT ,CHAWATA , Kilide , LHRC , AFP , GIYEDO ,Codert , WOINSIO , Individual Activists , TGFA -Wakulima , Haki Madini , Gender Training Institute(GTI), Kilide-KLD, Mama Ardhi Alliance (PWC,URCT,TAWLA,WLAC,Envirocare), VODIWOTA

		• Katiba mpya kwa kuweka dhahiri kuwa wanawake na wanaume ndio kwa pamoja wananchi, raia, na wanadamu wa Jamhuri ya Tanzania • Utangulizi ni sehemu muhimu ya Katiba ya nchi yetu - inaweka bayana dhamira ya Katiba: Kwa mfano, Rasimu ya Pili ya Katiba ni muhimu itamke kuwa.. ***sisi wananchi, wanawake na wanaume wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi…….kuzingatia misingi ya utu, uhuru na usawa…*** • Aidha pendekezo hili linatokana na kwamba mara baada ya kupata uhuru wimbo na nembo ya Taifa vilibaini wanawake na wanaume kuwa ndio kwa pamoja watnanchi wa Tanzania.
Ibara ya 5 (a, b, c, d, e, f, g) inataja Tunu za Taifa	Msinig wa usawa wa ijinsia kutotambulika kama mojawapo ya TUNU za Taifa	**Pendekezo:** Rasimu itambue na kuorodhesha Usawa wa ijinsia kama mojawapo ya TUNU za Taifa. **Hoja:** • Usawa wa ijinsia ikiwa mojawapo ya TUNU za Taifa itadhihirisha utashi wa nchi katika kutimiza maazimio ya kimataifa na kikanda yanayohusu usawa wa kijinsia. • Utambuzi wa tunu hiyo utaweka msingi wa kujenga Taifa linalojivunia usawa kati ya wanaume na wanawake kam muhimili mzuri wa maendeleo. • Aidha itaweka msingi wa kuwajibisha na kufanya wananchi twaache kudhalilisha na kubagua wanawake. Katika ngazi mbalimbali.
Ibara ya 6 (a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote	Kunakosekana utambulisho wa dhana ya wa wananchi kwa mrengo wa kijinsia	**Pendekezo:** Utambulisho wa Wananchi wa Tanzania utamkwe bayana kuwa **Wananchi, wanaume kwa wanawake ndio msingi wa mamlaka yote...**

		Hoja: • Utambulisho wa Wananchi wa Tanzania unahitaji sura ya mwanamke na mwanamme (kama ilivyo kwenye nembo ya taifa) . Hivyo ni muhimu Katiba iweke bayana kuwa Wananchi wa Tanzania ni wanaume na wanawake.
Ibara ya 10 (1) Lengo Kuu la Katiba hii ni kulinda, kuimarisha na kudumisha haki… **Ibara ya 10 (2)**)….lengo kuu litaendelezwa na kuimarishwa katika Nyanja za kisiasa, kijamii kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira.	Kutokuingiza ***usawa wa jinsia*** katika **Lengo Kuu la Katiba** Kutokuweka bayana msingi wa usawa wa jinsia kama lengo mojwapo litakalozingatiwa katika kutekeleza nyanja mbalimbali za maendeleo.	**Pendekezo:** Kuingiza msingi wa ***usawa wa jinsia*** katika Lengo Kuu la Katiba. **Isomeke:** "Lengo Kuu la Katiba hii ni kulinda, kuimarisha na kudumisha haki, usawa wa jinsia, udugu…." **Pendekezo:** Kuweka bayana dhamira ya kikatiba katika kufikia usawa wa jinsia katika utekelezaji wa malengo ya taifa ya: kisiasa, kijamii, kiuchumi, kuitamaduni na kimazingira. **Ibara ya 10 (2) isomeke:** "…lengo kuu litaendelezwa na kuimarishwa kwa ***kuzingatia usawa wa jinsia*** katika nyanja zote kuu, ikijumuhisha nyanja za kisiasa, kijamii kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira" **Hoja:** • Nchi huru ya Tanzania idhamirie kutambua na kukuza misingi ya usawa wa jinsia ili kudumisha maendeleo yanayowanufaisha wananchi wake wote, wanaume kwa wanawake na hata watoto. • Kutojumuisha usawa wa jinsia katika Lengo Kuu la Katiba kutapelekea kudhoofisha utekelezaji na uwajibikaji wa vyombo vya dola kuchukua hatua za makusudi za kurekebisha mapengo ya jinsia yaliyotokana na mfumo wa ubaguzi. • Kama Katiba imedhamiria kutoa ***fursa sawa*** kwa wanawake na wanaume kama ilivyoainishwa katika sura hii 7 (g), sharti hii dhamira ijitokeze kwenye Lengo Kuu la Katiba (10 (i) ili kuongoza utekelezaji utakaozingatia usawa wa jinsia katika nyanja za siasa, uchumi, utamaduni mazingira na ustawi wa jamii kwa ujumla.

		• Tanzania imeridhia Tamko la AU kuhusu usawa wa Jinsia (African Union Solemn Declaration on Gender Equality in Africa 2004). Hivyo ni muhimu Katiba ambayo ni sheria kuu au sheria mama, iweke misingi itakayowajibisha serikali na vyombo vyake kutekeleza mikataba na matamko ya kimataifa na kikanda, hususan ni haki za wanawake. **Mfano wa Katiba Iliyoainisha usawa wa Jinsia kama Lengo Muhimu (Katiba ya Malawi).** *Misingi ya Sera za Malawi: " Serikali ya Malawi inadhamiria kushughulikia ustawi wa jamii na maendeleo ya watu wote kwa kuweka sera na mipango endelevu pamoja na sheria ili kuhakikisha kwamba; (a) kufikia usawa wa jinsia kwa wanawake na wanaume kwa kuzingatia; (i) ushiriki wa wanawake katika Nyanja zote za jamii kwa kuzingatia usawa kati ya wanaume na wanawake (ii) kutekeleza msingi wa kutokubagua kwa kuchukua hatua za makusudi za kurekebisha tofauti zilizoko (iii) kutekeleza sera za jamii zitakazoshughulikia masuala ya ukatili wa jinsia, usalama wa raia, haki za likizo ya uzazi, kupambana na sera za unyonyaji wa uchumi na haki za umiliki mali (tafsri)".*
Ibara ya 10 (c) Kiuchumi	**Ibara ya 10** (c) (i)-(xiii) Vipengele hivi viko kimya kabisa kuhusu mchango wa wanawake katika Uchumi wa Taifa na Jukumu la Serikali katika kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake.	**Pendekezo:** Serikali ionyeshe dhamira ya kujenga mfumo mbadala na kuweka mazingira bora ya kisera ya malezi na matunzo yatakayowezesha wanawake na wanaume kushiriki na kuchangia katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayo walemea wanawake na watoto wa kike. **Hoja:** • "Care economy" ni shughuli za jamii za malezi na matunzo zinazofanywa na wanawake, watoto wa kike na makundi yaliyo pembezoni, zikiwepo zile za nyumbani, kazi za kulea watoto, kutunza wazee na wagonjwa wanaorudishwa nyumbani (wengi wakiwa ni wagonjwa wa UKIMWI). • Japo hizi shughuli hazionekani dhahiri katika michakato ya uchumi mkuu na sera, hakuna budi kutazitambua kikatiba kwa kuwa zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi mkuu.

- Aidha ni muhimu kutambua kuwa shughuli za malezi ya watoto wanazofanya wanawake ni mchango mkubwa katika kuzalisha ***rasilimali watu ya taifa.***

Savei ya matumizi ya muda ya 2006 ilitambua umuhimu wa mchango huu wa "care economy"

- Taarifa na takwimu sahihi za "care economy" Tanzania zilizalishwa na savei ya Shirika la Taifa la Takwaimu (National Bureau of Statistics –NBS) mwaka 2006.
  - Mwaka 2006 NBS waliingiza moduli ya matumizi ya muda (time use) katika Savei ya Nguvu Kazi (Integrated Labour Force Survey –ILFS).
  - Hii moduli ilitathimini jinsi Watanzania wanavyotumia muda wao katika shughuli za nyumbani kila siku. Shughuli zilizoangaliwa ni zile ambazo hazilipwi, zikiwepo za kuteka maji, kutafuta kuni, kulea watoto, kutunza wazee na wagonjwa wa UKIMWI.
  - Utafiti ulionyesha kuwa wanawake wanafanya kazi zisizolipwa kuliko wanaume. Katika Utafiti huu wanawake walionekana kufanya zaidi ya robo tatu ya kazi zote za nyumbani, kulea watoto na kutunza wagonjwa.
  - Aidha utafiti ulionyesha kuwa kazi hizo wazifanyazo wanawake ni mzigo mkubwa kwao kiasi kwamba huweza kuwanyima fursa sawa ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji na hata za siasa.
  - Utafiti pia ulizithaminisha kazi za malezi kuwa sawa na asilimia 63 ya Pato la Taifa (GDP) la mwaka 2006.

		• Hivyo kwa kutokutambua "care economy" katika Katiba ni kuacha kutambua mchango mkubwa wa wanawake na makundi yaliyo pembezoni katika uchumi mpana wa Taifa na hivyo kutokuwapa watoa mchango huo motisha za kisera ipasavyo, na hata kutoelekeza rasilimali fedha na watu katika kuboresha shughuli wazifanyazo manyumbani na kwingineko.
Ibara ya 23 (1) Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa.	Msingi huu wa usawa wa jinsia hauku-gusiwa katika maeneo mengine ya Rasimu hii isipokuwa tu katika ushiriki wa wanawake katika Bunge la Muungano…	**Pendekezo:** Msingi wa usawa huu wa jinsia uongoze vipengele vingine vya Katiba vinavyohusiana na uongozi na mamlaka ya vyombo vya dola katika ngazi mbalimbali. **Hoja:** • "Ongezeko la uwakilishi wa wanawake kutoka majimbo ya uchaguzi umekuwa ukiongezeka kwa kasi ndogo mno ukilinganisha na idadi ya wanawake katika nchi yetu ambao ni takribani asili mia 51%. • Mifano mizuri ya Bunge Maalum la Katiba imeonyesha kuwa utekelezaji wa msingi wa uwiano wa jinsia katika uongozi na maamuzi muhimu ya kitaifa inawezekana. Hivyo basi itam-kwe wazi kabisa katika Katiba mpya kuwa katika kila uteuzi lazima msingi wa usawa wa jinsia uzingatiwe, na hasa uteuzi katika nafasi za: ***Rais (ME) – Makamu (KE); Jaji Mkuu (ME) – Naibu (KE); Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufaa, Spika wa Bunge*** Uhalali wa pendekezo hili unatokana na kuwepo kwa wanawake wananchi ambao ni asilimia 51% ya Watanzania na kwa kuzingatia kuwa ndio wazalishaji wakuu nchini Aidha kuwepo viongozi wanawake waadilifu katika nafasi za maamuzi kunaweza kuleta faida zifuatazo: • Viongozi wanawake katika nafasi zao watatoa msukumo kwa masuala ya wanawake, wasichana, wanawake wenye ulemavu na usawa wa jinsia;

		• Viongozi wanawake watalinda rasilimali ya Taifa isiporwe na kuhakikisha ralisimali za nchi zinaelekezwa katika kutekeleza haki za wanwake zilizoainishwa katika Katiba. Wanawake wakiwa wananchi wa nchi hii wana uwezo mkubwa wa kutoa msukumo kwa mipango na mikakati itakayoelekeza rasilimali za taifa katika kujenga jamii yenye ustawi na usawa wa jinsia.
Ibara ya 37 (1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na hifadhi ya mali yake.	Ibara iko kimya kuhusu haki za mwanamke kumiliki mali na kupata hifadhi ya mali yake.	**Pendekezo: Ibara ya 37 (1)** itamke bayana kuwa wanawake wana Haki ya Kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika ikiwemo ardhi ya ukoo; Haki ya kurithi; Haki ya kugawana sawa mali ya ndoa, n.k. **Hoja:** • Wanawake ni asilimia 80% ya nguvu kazi vijijini na asilimia 60% ni wazalishaji wakuu wa chakula na mazao ya biashara. • Utafiti uliyofanywa mwaka 2012 na Oxfam unaonyesha kwamba ni takribani asilimia 5% tu ya wanawake wanaofanya kazi za kilimo wenye kumiliki ardhi yao, asilimia 44% wanafanya shughuli za kilimo kwenye ardhi inayomilikiwa na waume zao, na asilimia 35% wanafanya kazi kwenye ardhi inayomilikiwa na ukoo. Na katika utafiti huu, wanawake 2 kati ya 3 walikiri kwamba kunyimwa haki ya kumiliki ardhi wanayoifanyia kazi kunadumaza maendeleo yao na ya familia zao.(chanzo: Dailynews.co.tz/index/php/feature/24296-tanzania).
Ibara ya 42 (1) (b): Kupata elimu bora ya msingi bila ya malipo na inayomtayarisha kikamilifu mwanafunzi ama	Ibara 42 (1) (a) (b) (c) (d) haitambui mazingira yasiyo wezeshi kwa msichana na ubaguzi wa jinsia kama vikwazo vinavyomkwamisha fursa sawa ya elimu hasa kwa watoto wa kie.	**Pendekezo: Ibara 42 (1) Isomeke *"Kila mtu ana haki ya: (a) kupata elimu bora bila vikwazo hadi kidato cha nne"*** **Ibara 421) (d) Isomeke – *haki ya kupata elimu ya juu izingatie msingi wa usawa ili mradi ana sifa stahiki kupata elimu hiyo, bila ya ubaguzi wa aina yoyote.***

kuendelea na elimu ya ngazi inayofuatia au kuweka msingi wa kuanza kujitegemea..

Ibara 42 (1) (d) kupata fursa sawa ya kupata elimu ya juu ili mradi ana sifa stahiki kupata elimu hiyo, bila ubaguzi wa aina yoyote.

Dhanaya fursa haiwajibishi serikali kuwapatia watoto wa kike nafasi ya elimu.

Nyongeza:
Katiba ielekeze wazi uwepo wa mfumo wa elimu unaozingatia usawa wa jinsia, na kujengea mazingira salama na rafiki ya kumuwezesha mtoto wa kike kupata elimu bora kuanzia elimu ya msingi hadi chuo (empowering of the girl child)

Hoja:

- Takwimu: *Takriban 39.5% ya wanawake hawajasoma ukilinganisha na asilimia 25.3% ya wanaume ambao hawajasoma. Taarifa ya BEST 2010 ilionyesha kuwa mwaka 2009 theluthi moja 1/3 tu au 32.1% ya wanafunzi wote wa vyuo vikuu walikuwa wanawake (yaani 20,083 kati ya wanafunzi 70,785)*

Elimu ya msingi ya darasa la saba haina manufaa kwa mtoto

- Kwa mazingira ya sasa, elimu ya msingi ya kuishia darasa la saba haitoshelezi. Mwanafunzi awe wa kike au wa kiume, anakuwa bado hajaweza kujitegemea.
- Hususani, kwa mwanafunzi wa kike anapomaliza darasa la saba (wengi wakiwa miaka 14 na 15) pamoja na uwezo mdogo wa kujitegemea, anaozwa kutokana na fikra za baadhi ya jamii kuwa anaweza kuleta aibu ya kupata mimba.
- Kwa kumpatia msichana nafasi ya kusoma hadi kidato cha nne na hata katika ngzai za juu zaidi, ataepuka kuozwa katika umri mdogo na anapewa nafasi ya kufanya maamuzi ya busara kuhusu maisha yake na ya kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Uhusiano wa elimu na rasilimali ya taifa:

- Tafiti zinaonyesha kwamba baadhi ya nchi hupoteza zaidi ya dola bilioni moja kwa kushindwa kusomesha watoto wa kike.
- Kwa kuwawekea watoto wa kike mazingira ya kufikia na kufaidi elimu utaimarisha rasilimali watu ya taifa.

		Elimu ni haki ya mtoto: • Tanzania imeridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Watoto (CRC) ambao umeweka bayana haki za watoto wa kike katika kufikia na kufaidi. • Kwa Tanzania lengo la 3 la Milenia na lengo la 5 la Elimu Sawa kwa Wote (EFA) yalidhamiria kutokomeza mapengo ya kijinsia katika elimu na kufikia usawa wa kijinsia katika elimu ifikakapo mwaka wa 2015. Hata hivyo malengo haya haya-jafanikiwa kuleta usawa wa kijinsia katika sekta ya elimu kwa sababu hatujaweza kukabiliana na vikwazo vya kimfumo (vinavyojilkta kwenye ubaguzi, fikra mgando, mila na desturi kandamizi na umaskini) vinavyokwamisha elimu ya wasi-chana. Katiba mpya lazima ielekeze uwepo wa mkakati wa kimapinduzi wa kutekeleza haki za mtoto wa kike na uwiano wa kijinsia.
Ibara ya 43 (2) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha utekelezaji na usimamizi wa haki za mtoto kwa kufuata msingi wa kutoa kipaumbele kwa maslahi na manufaa ya mtoto.	• **Ibara ya 43** iko kimya kuhusu haki za Mtoto wa kike, ulinzi na usalama wake • Katiba haijamuwekea mtoto wa kike mazingira yatakayomsaidia kupata haki zake zote kama ilivyo kwa mtoto wa kiume. • Aidha inakosekana tafsri ya mtoto.	**Pendekezo: Ibara ya 43 (2)** Isomeke-Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha utekelezaji na usimamizi wa haki za mtoto, husuani mtoto wa kike, kwa kufuata msingi wa kutoa kipaumbele kwa maslahi na manufaa ya mtoto. Tafsri ya mtoto isomeke: **Mtoto ni msichana au mvulana aliye chini ya umri wa miaka 18.** **Kiongezwe kifungu kidogo (4)** Mamlaka ya nchini itaweka utaratibu utakaomlinda mtoto wa kike dhidi ya mazingira ya kubaguliwa, kunyanyapaliwa, na vitendo vya ukatili kama vile kukeketwa, ndoa za utotoni, haki ya kurithi na ain azote za unyanyasaji. **Hoja:** Tanzania imeridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za watoto (CRC) ambao umeweka bayana haki za watoto wa kike katika kufikia, kufaidi elimu, ulinzi wa watoto wa kike dhidi ya mila na desturi kandamiza, haki sawa za kurithi mali za wazazi, kulindwa dhidi ya vitendo vyo vyotevya udhalilishaji ikiwa ni pamoja na biashara ya ngono, ukeketwaji, ndoa za utotoni na ubakaji.

Ibara 44: Kila kijana ana haki na wajibu wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Jamhuri ya Muungano pamoja na jamii kwa ujumla…

Hii siyo hali halisi na hivyo kunakosekana mazingira yatakayowawajibisha vijana ili wasijiingize katika wizi, madawa ya kulevya na shughuli zingine ambazo ni kinyume na maadali ya taifa...

Aidha kunakosekana dhana kunyambuliwa kijinsi ili kuonyesha ke and me na pia kuonyesha kuwa jinsi zote mbili zitashiriki na kufaidi (fursa na haki sawa; kuwa na usawa katika kufikia na kumiliki rasilimali na usawa katika ulinzi.

Pendekezo: Kiongezwe kifungu/kipengele: Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunga sheria itakayobainisha haki na wajibu wa kijana katika kujiletea maendeleo.

Hoja:

- Haki hii imewekwa katika Katiba kwa mara ya kwanza kwa kutambua vijana, wa kiume au wa kike, kama nguvu kazi kuu ya taifa. Sensa ya 2012 imeonyesha kuwa vijana ndio kundi kubwa zaidi la Watanza nia kwa asilimia 60.
- Haki na wajibu wa vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo itatoa matunda tu pale vijana, wa kike na wa kiume, watakpopewa mazingira wezeshi kaitka ngazi mbalimbali ili wajitume na kutambua wajibu wao katika maendeleo ya taifa na wa kujiletea maendeleo yao wenyewe.
- Ni muhimu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuweka mfumo wa sheria utakaohakikisha kuwepo kwa mazingira yatakayowawajibisha vijana kujiletea maendeleo na kuacha kujiingiza katika vitendeo vya wizi, madawa ya kulevya na shughuli zingine ambazo ni kinyume na maadali ya taifa.

Pendekezo: Elekeza dhana kunyambua vijana kijinsi ili kuonyesha ke and me watakvyoshiriki, kufaidi fursa na haki zao.

Ongeza: ***Vijana kufaidi fursa na haki sawa; kuwa na usawa katika kufikia na kumiliki rasilimali na usawa katika ulinzi.***

Hoja:

- Vijana ke na me wanahitaji kuwepo kama washilriki na wadau wakuu wa kuleta maendeleo ya nchi hii na pia kuwa wananchi wanaostahili haki na fursa sawa ya kufikia na kumiliki mali na kupata ulinzi katika ngazi mbalimbali.

Ibara 45 (1): Mtu mwenye ulemavu anastahiki:

(a). kuheshimiwa, kutambuliwa na kutendewa kwa namna ambayo haishushi utu wake.

(b). kuwekewa miundo mbinu na mazingira yatakayowezesha kwenda anapotaka, kutumia vyombo vya usafiri na kupata habari;

Ibara iko kimya kuhusu haki za wanawake wenye ulemavu.

Aidha kuna upungufu wa maelezo yanayolenga mazingira rafiki kwa ajili ya afya bora ya mwanamke mwenye ulemavu.

Pendekezo: Kiongezwe kifungu/kipengele: Ibara ya 45 itamke bayana haki za wanawake wenye ulemavu zikiwemo:

- Kutokubaguliwa katika ajira
- Haki ya kufikia huduma za jamii kama vile elimu, afya na huduma nyinginezo kwa kuhakikisha kuwepo mazingira wezeshi kwa mtoto wa kike/mwanamke mwenye ulemavu.
- Haki ya kupatiwa huduma za uzazi salama kwa kuzingatia hali ya ulemavu wao.
- Haki ya kulindwa kutokana na vitendo vya kikatili dhidi yao.
- Haki ya kushiriki katika ngazi za maamuzi na uongozi

Aidha Ibara itamke kuwa kutakuwepo na sheria zitakazowalinda wanawake walemavu dhidi ya vitendo vya unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na kubaguliwa.

Hoja:

- Wanawake wenye ulemavu hupata changamoto nyingi za kipekee tofauti na wanaume wenye ulemavu. Mara nyingi wanadhalilishwa kwa vitendo vya ukatili kama vile kubakwa, kunyanyaswa kijinsia, kubaguliwa na kunyanyapaliwa. Vitendo hivi vinashusha utu wa mwanamke mwenye ulemavu nchini kwake.
- Asilimia 4% tu ya watoto wenye ulemavu wanasoma mashuleni. Idadi ya watoto wa kike wenye ulemavu mashuleni ni ndogo ikilinganishwa na wavulana katika ngazi zote. Kutokana na takwimu hizi, ushiriki wa watu wenye ulemavu katika ajira rasmi ni mdogo wengi wako katika ajira isiyo rasmi au hawana ajira. Wengi wanategemea kuomba misaada.
- Huduma zote za kijamii nchini (elimu, afya, ajira, barabara na usafiri, majengo, taarifa /mawasiliano n.k) bado hazijazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu; aina ya ulemavu na masuala ya kijinsia katika ulemavu

		• Kutokana na mitizamo ya jamii, wanawake wenye ulemavu hawana nafasi sawa za kuingia katika mahusiano rasmi ya ndoa ikilinganishwa na wanaume. Kwa sababu hii wengi wanalea familia zao wenyewe huku wakiwa hawana umiliki wa rasilimali, elimu, ajira , taarifa n.k • Rasimu ya Katiba imetambua Utu wa Mtu kama msingi muhimu wa Haki za Binadamu Ibara ya 23 (2) " Kila Mtu anayohaki ya kuheshimiwa, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake" na Ibara ya 47 (1)(a) Kila Mwanamke ana haki ya Kuheshimiwa Utu wake
Ibara ya 47 (1) (a-g) na **(2)** inazungumzia haki mbalim-bali za wanawake	Katika kubainisha haki mahsusi za wanawake, baadhi ya haki za msingi za wanawake hazikuguswa.	**Pendekezo:** • Haki za wanawake zipanuliwe kwa kuongeza: • Haki ya mwanamke kumiliki mali iliwepo ardhi; kurithi mali ya wenza wao; • Haki ya uzazi salama; • Haki ya kulindwa dhidi ya vitendo vya kikatili; • Haki ya faragha kwa wale walioko kizuizini, na adhabu zinazolingana na hali zao iwapo ni wajawazito. • Haki sawa ya kushiriki uongozi katika ngazi zote; • Haki ya kutobaguliwa (katika elimu, ajira, na kipato) • Haki ya maisha salama kwa wanawake wazee ambao wana uwawa kwa imani za kishirikina **Hoja:** • Huwa hakuna tabaka katika haki za binadamu- hadhi sawa kwa haki zote za uraia, utamaduni, uchumi, siasa na kijamii. • Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa na ya kikanda (mf CEDAW, Protokali ya Makubaliano ya Haki za Binandamu ya Umoja wa Afrika–Protokali ya Maputo) ambayo ikiwekewa sheria, sera na mipango itakukuza upatikanaji wa haki za wanawake.

		• Haki za binadamu ni thamani halisi inayompa binadamu utu. • Tamko la Vienna la Haki za Binadamu (1993) lilitamka kwamba haki zote, za wanawake au wanaume, zina hadhi sawa. • Aidha Tamko la Vienna la haki za Binadamu lilitamka kuwa haki za wanawake ni haki za binadamu. • Serkali ndiyo mhusika mkuu (principal duty bearer) wa kutoa haki kwa wanawake na watoto wa kike na wajibu wa serikali katika kutoa haki kwa watu wake- Dhana ya ulinzi huu wa kisheria uonyeshwe dhahiri katika Katiba ya nchi.
Ibara ya 47 (1): Kila mwanamke ana haki ya: (g) kupata huduma bora ya afya	Ibara haibaini kwa ufanisi msingi wa hai ya uzazi salama hasa kwa wanawake	**Pendekezo: Kiongezwe kifungu kidogo (h)** kitakachomwezesha mama mjamzito kupata huduma bora ya afya ikiwa ni pamoja na ya uzazi katika eneo analoishi. Zaidi ya hapo wanawake walezi wapatiwe bima ya afya kwa gharama za serikali mpaka mtoto atakapofikia umri wa miaka mitano. **Hoja:** • Haki ya Uzazi Salama ni msingi muhimu katika kupunguza vifo vya wanawake na wasichana. • Afya ya uzazi salama ufanywe msingi muhimu katika Katiba Mpya kuonyesha dhamira ya serikali/nchi katika kutetea haki za wanawake kwa ujumla. Msingi huu ni muhimu sana kwa taifa kwani wanawake wanapokuwa na afya na usalama wa maisha yao, watajifungu watoto wenye afya, na hivyo kuwezesha taifa kuwa na raslimali watu wenye afya. • Vifo vya wanawake katika uzazi ni ukiukwaji wa haki yao ya kuishi, na vile vile ni gharama kwa taifa. Takribani wanawake 432 kati ya kila wanawake 100,000 wanaojifungua hupoteza maisha yao kwa mwaka. Hii ni hasara kubwa katika ngazi ya binafsi, jumuiya na serikali/kitaifa.

		• Ni asilimia 46% tu ya wanawake wa Tanzania ambao wana-pata huduma ya kujifungulia hospitalini na kuhudumiwa na wataalam wa afya. Kuna tofauti kubwa sana ya huduma hizi katiyna miji na vijiji na kati ya kaya zenye uwezo na zile masikini. Wengi wanaopoteza maisha wako, vijijini kutokana na umbali wa vituo vya afya, kulipia gharama za uzazi, ufinyu wa watoa huduma wenye ujuzi vijijini, vifaa /vitendea kazi; uelewa finyu na mzigo wa kazi kwa wanawake wajawazito.
Ibara ya 47 (1) Kila mwan-amke ana haki ya: (e) kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu na mila zenye mad-hara;	Kumekosekana kipengele cha kusistizwa haki ya mwanamke katika kulindwa dhidi ya ukatili wa jinsia-zikiwemo ukatili wa udhalilishaji kingono, n.k.	**Pendekezo:** Ongeza kipengele cha haki ya mwanamke kulindwa dhidi ya ukatili wa jinsia **Ibara ya 47 (1) isomeke: Kila mwanamke ana haki ya:** (e) kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu, mila zenye madhara na ukatili wa kijinsia kwa ujumla **Hoja:** Historia yenye misingi ya ubaguzi wa jinsia, mila na desturi zinazokandamiza ukiwemo mfumo dume zimechangia katika ukatili wa jinsia ambao ni kinyume na haki za binadamu. **Hali ya ukatili wa kijinsia nchini:** • Utafiti wa Afya ***(Demographic Health Survey)*** 2010 ulibanini kuwa theluthi moja (1/3) au asilimia 30%) ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 nchini Tanzania wanafanyiwa ukatili wa kijinsia (kimwili) kila mwaka ukiwemo vipigo, ubakaji, mauaji , saikololia (DHS 2010) • Asilimia 44% ya wanawake wote walioolewa wamefanyiwa ukatili wa kijinsia(kimwili) • Asilimia 15% ya wanawake wa Tanzania wamefanyiwa tohara. • Aidha kuna ukatili dhidi ya wanawake wazee (kuuawa kwa imani ya kishirikina) na wanawake kukukutana na rushwa ya ngono

		Tanzania imeridhia Mikataba ya Kikanda na ya kupinga ukatili wa kijinsia Ikiwepo: • Mkataba wa Kimataifa kuhusu kutokomeza aina zozote za ubaguzi dhidi ya wanawake (Convention on the Elimination of al Forms of Discrimination Against Women (CEDAW) 1979. • Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia ukatili na aina zote za dhuluma dhidi ya binadamu (Convention against Torture and other cruel, inhuman or degrading treatment or punishment) 1984. • Tamko la Beijing na Mpango Kazi (Beijing Declaration and Platform of Action) 1995. • Protokali ya Kuzuia, na kutokomeza biashara ya watu, husasani wanawake na watoto (Protocol to Prevent, Suppress and Punish trafficking of persons, especially women and children) 2000. • Protokali ya Makubaliano ya AU kuhusu haki za binadamu na haki za wanawake (The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of women 2002). • Tamko la AU kuhusu usawa wa Jinsia (African Union Solemn Declaration on Gender Equality in Africa) 2004.
	Aidha Rasimu haikuweka bayana umuhimu wa kuunda chombo kitakachoshughulikia ulinzi wa haki za Wanawake (Commission for Gender Equality) nchini.	**Pendekezo: Ongezeko kwa kifungu (3) Isomeke:** Utaratibu utawekwa wa kuunda Tume itakayosimamia ufuatiliaji na usimamizi wa haki za wanawake na usawa wa jinsia nchini. **Hoja:** • Msingi wa usawa wa jinsia unastahili kuendelea kupiganiwa na kuwekewa mfumo wa utekelezaji na usimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto wa kike nchini. • Ni muhimu basi, Katiba Mpya ikaweka bayana umuhimu wa kuunda chombo cha kiatifa kitakachoshughulikia ulinzi wa haki za Wanawake (Commission for Gender Equality) nchini. ○ **Kwa mfano, Katiba ya Kenya** *imebainisha kuundwa kwa Tume ya Haki za binadamu – Human Rights Commission and Equality ambayo moja ya jukumu lake ni kusimamia utekelezaji wa haki za wanawake.*

Ibara 47 (2) …..usalama na fursa za wanawake wakiwemo wajane	Dhana ya **fursa** linatoa mwanya wa kutowajibika kwa serikali kwa makundi haya.	**Pendekezo:** Badala ya kutumika kwa dhana ya **fursa** itumike dhana ya **HAKI – Isomeke…usalama na haki za wanawake wakiwemo wajane.**
		
		Hoja:
		• **Kwa nini misingi ya haki badala ya fursa kwenye Katiba?**
		  ○ Fursa huweza ikatolewa au isitolewe bali haki ya mtu anazaliwa nayo.
		  ○ Haki haiwezi kutenguliwa au kuchukuliwa.
		  ○ Haki hufanana na ni sawa kwa binadamu wote ulimwenguni

Ibara 48…Mamlaka za nchi zitaweka utaratibu utakayowezesha wazee kupata fursa ya….	Kutokubainisha kwa wanawake wazee kama kundi ambalo haki zao zipo hatarini. Kutumia kwa dhana ya fursa badala ya **haki…….Dhana ya HAKI badala ya fursa??**	**Pendekezo:** Ibara itamke bayana kuwa wanawake wazee wana haki ya kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyowalenga wao. Na pia wana haki sawa za kupata hifadhi ya jamii na matunzo bora **Hoja:** • Pamoja na kuwa wanawake wa vijijini ndio wazalishaji wakubwa, hali halisi inaonyesha kuwa wakiwa wazee hali zao huwa mbaya kutokana na wao kuishi maisha ya umaskini. • Aidha wanawake wazee hukosa hifadhi ya jamii na matunzo bora na ni kuwakosea haki na kuwaacha katika hali hatarishi (vulnerable). • Takwimu zinaonyesha kuwa ni wanawake wazee tu huuwawa kwa kushukiwa ni wachawi. Ni nadra kukuta wanaume wazee wakinyooshewa kidole kuwa ni wachawi. • Kulingana na Ripoti ya mwaka wa 2009 iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, takriban jumla ya mauaji ya wanawake wazee 2,585 yaliripotiwa kati ya mwaka 2004 hadi 2009 katika mikoa ambamo matukio hayo yameshamiri. Takwimu hizi zina maana kuwa ni wastani wa mauji 517 kwa kila mwaka. Mkoa wa Mwanza ambao unaongoza kwa mauji ya wanawake wazee ilikuwa na idadi ya mauji 698. Wengi wa hao waliouwawa walisingiziwa kuwa ni wachawi!

Sura ya 7, 9, na **10:** Uteuzi wa uongozi wa Juu wa Jamhuri ya Muungano pamoja na mihimili mikuu ya utawala.

- **Ibara ya 72 3(c)** bayana usawa wa jinsia kama sehemu ya majukumu na uwajibikaji wa Kiongozi wa juu wa nchi- Rais

- Uteuzi wa uongozi wa Juu wa Jamhuri ya Muungano pamoja na mihimili mikuu ya utawala, haukujikita katika msingi wa kulta usawa wa jinsia

Pendekezo: Ni muhimu kutetea kwa nguvu zote Ibara 113 (3) inayohusu usawa wa jinsia katika uongozi wa siasa ngazi ya bunge **(50/50)** ili kuhakikisha kuwa ***katika kila jimbo la uchaguzi kutakuwa na nafasi mbili za ubunge, moja kwa ajili ya mwanawake na moja kwa ajili ya mwanaume.***

Dhamira ya kuongeza ushiriki wa wanawake bungeni upanuliwe wigo ili uhusishe ngazi zote za uongozi nchini. Usawa wa Jinsia utumike katika kuongoza uteuzi wa viongozi kama ilivyoainishwa katika Katiba hii.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawajibika kuzingatia usawa wa jinsia katika uteuzi wa viongozi wa ngazi za juu kama ilivyobainishwa katika Tamko la AU kuhusu 50/50 (Tanzania imeridhia). Hii ikiwa ni pamoja na uteuzi wa baraza la mawaziri, na manaibu, makatibu wakuu, wakurugenzi na manaibu, msajili ya vyama vya siasa, uongozi wa vyombo vya uwajibikaji ikiwa ni pamoja na: Tume ya maadili ya Viongozi, Tume ya Haki za Binadamu, Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hata uteuzi wa tume huru ya uchaguzi.

Hoja:

- Ushiriki wa wanawake katika uongozi na ngazi za maamuzi ni haki yao ya kimsingi kama raia, hasa ikizingatiwa kuwa idadi ya wanawake katika nchi yetu ni takribani asilimia 51%,
- Rasimu imeweka bayana uwiano wa asilimia 50/50 katika uchaguzi wa wabunge Ibara ya 113. Msinigi huu wa uwiano wa jinsia ukipitishwa na bunge maalumu utapelelekea Tanzania kufikia kiwango kilichokubaliwa na nchi wanachama katika Protokali ya SADC na Tamko la AU.
- Hali ya ushiriki wa wanawake katika uongozi bado ni mdogo nchini. Pamoja na kuwepo na juhudi za kuongeza ushiriki wa wanawake katika maeneo/sekta/sehemu mbali mbali za maamuzi na uongozi, bado ushiriki wao ni mdogo ukilinganishwa na ule wa wanaume.

		◦ Mfano katika Bunge la 2010 -2015 asili mia 36% ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ni wanawake (126 kati ya wabunge 350). ◦ **Aidha** Kati ya Madiwani wa Halmashauri za serikali za mtaa 3,335, wanawake ni 1,272 tu ambo ni asilimia 30.6% ya madiwani wote. • Tanzania imesaini mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda inayokutetea usawa wa jinsia katika uongozi wa siasa na ngazi za uamuzi mfano: ◦ Tamko la Kimataifa kuhusu haki za Binadamu (Universal Declaration of Human Rights (1948). ◦ Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za raia na siasa (International Covenant on Civil and Political Rights ICCPR) (1966). ◦ Makubaliano ya Afrika kuhusu Haki za binadamu (African charter on Human and People's Rights (1981). ◦ Mkataba wa Kimataifa kuhusu kutokomeza aina zozote za ubaguzi dhidi ya wanawake (Convention on the Elimination of al Forms of Discrimination Against Women CEDAW (1979). ◦ Tamko la Beijing na Mpango Kazi (Beijing Declaration and Platform of Action) 1995. ◦ Protokali ya Makubaliano ya AU kuhusu haki za binadamu na haki za wanawake (The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of women 2002). ◦ Tamko la AU kuhusu usawa wa Jinsia (African Union Solemn Declaration on Gender Equality in Africa 2004).
Sura ya 11: utumishi wa Umma Sehemu ya Tatu .	**Ibara ya 184** Kanuni ya Usawa wa Kijinsia haikuzingatiwa kama msingi muhimu wa utumishi wa Umma	**Pendekezo:** Ibara ya 184 Kanuni ya Usawa wa jinsia iongezwe kama msingi muhimu wa utumishi wa Umma

Ibara 197 – Ibara hii haijazingatia misingi ya kuongoza vyama vya siasa, kanuni za usajili, uwakilishi wa wananchi, Tume huru ya Uchaguzi, Msajili wa vyama vya siasa kubeba au kuwajibishwa katika kujenga kikatiba usawa wa kijinsia.

Utumishi wa umma na usio wa umma, uongozwe na misingi ya kuleta fursa sawa kati ya wanawake na wanaume (equal opportunity principles) na vile vile uongozwe na misingi ya ujenzi wa usawa wa jinsia ulioimarika (gender equality principal).

Hoja:

- Tanzania imeridhiria kwa hiari, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Kutokomeza Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW: 1985) na Mkataba wa AU (Maputo Protocal 2007) – mikataba ambayo inawajibisha wanachama wake kutekeleza makubaliano hayo kwa kuweka sheria, sera, taratibu/kanuni na mipango itakayoendana na makubaliano yaliyoko kwenye mikataba hiyo.

Pendekezo: Ibara 197 – Vyama vya siasa, kanuni za usajili, uwakilishi wa wananchi, Tume huru ya Uchaguzi, Msajili wa vyama vya siasa: vijazingatie na kulinda misini ya usawa wa insia

Hoja:

- Ni muhimu msingi wa asilimia 50/50 katika uongozi uendelezwe katika ngazi zote nchini na siyo kwenye ngaziya Bunge tu.
- Kushiriki katika uongozi wa siasa katika nchi ni haki ya Kikatiba ya kila raia.
- Pamoja na ushiriki katika uongozi/maamuzi muhimu ya taifa kuwa haki ya wanawake bado kuna mawazo mgando kuwa siasa ni eneo/uwanja wa wanume. Haya yatatoka tu endapo Katiba mpya itaendelea kubainisha raia wote wana haki sawa ya uraia, siasa na haki katika uchaguzi.
- Aidha nchi inawajibika kutekeleza mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda iliyosaini kuhusianan na usawa katika haki za uraia na siasa.

Sura ya 13: Taasisi za uwajibikaji	**Pengo:** Kukosekana kwa Taasisi za Uwajibikaji kwa masuala ya haki za wanawake na kulinda utekelezaji wa usawa kijinsia.	**Pendekezo: Katiba Mpya** itamke bayana kuanzishwa kwa Chombo maalum cha kitaifa kusimamia na kuhakikisha usawa wa jinsia kikatiba *(Commission for Gender Equality)*. **Hoja:** • Bila kuwa na mfumo wa kuwajibisha serikali na vyombo vyake vyote kutekeleza sera, sheria na mipango inayozingatia misingi ya usawa wa jinsia unaotambuliwa Kikatiba itakuwa vigumu kufikiautekelezaji na uwajibikaji katika suala la usawa wa jinsia kama eneo muhimu la maendeleo nchini. • Tanzania kama nchi, imekuwa na dhamira ya kuondoa ubaguzi wa jinsia lakini matokeo yamesua sua kwa sababu ya kukosa Chombo huru cha kuwajibisha serikali na watekelezaji wake kuonyesha matokeo yenye mwelekeo wa kijinsia. **Afrika ya Kusini na Kenya ni mifano ya nchi zenye Commission for Gender Equality:** Hiki ni chombo kilichowekwa Kikatiba kukuza na kuimarisha demokrasia na utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu katika nch, zikiwemo haki za wanawakei. Jukumu la Commission ni kukuza usawa wa jinsia katika nyanja zote za jamii na kutoa mapendekezo ya sheria zote zinazoathiri hali ya wanawake nchini.
Sura ya 14: Masharti kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano	**Pengo:** Rasimu iko kimya kuhusu uwajibikaji wa serikali na vyombo vyake katika kutenga fedha za kushughulikia uletaji, ulindaji wa haki na matokea ya maaendeleo yenye mrengo wa kijinsia	**Pendekezo:** Katiba itamke bayana kuwa kutakuwepo na uwazi, uwajibikaji na ushiriki (there shall be openness and accountability including public participation) wa wanawake na wanaume katika ugawaji wa rasilimali za taifa, ikiwemo bajeti ya taifa... Aidha, Katiba itamke bayana kuwa mchakato wa bajeti ya taifa utarasimisha uandaaji wa bajeti kwa MRENGO WA KIJINSIA na kwamba zitawasilishwa pamoja na Tamko la Bajeti Kijinsia katika bunge la Muungano na katika ngazi ya Halmashauri nchini...

	Pengo: Masharti hayakugusa umuhimu wa matumizi ya fedha za Jamhuri kuzingatia misingi ya usawa ikiwemo usawa wa kijinsia, uadilifu, uwazi na ushiriki wa umma.	**Hoja:**
		• Fedha za umma zielekezwe kwenye ujenzi wa misingi ya usawa, ikiwemo usawa wa jins ndani ya jamii (the public finance system shall promote equitable society) na hususani:
		  ◦ Kodi iwekewe misingi ya usawa wa kijinsia na utoaji wa haki kwa wanawake (the burden of taxation shall be shared fairly with a special focus of promoting women's rights;)
		  ◦ Pato la taifa litumike kwa kuzingatia misingi ya usawa wa kijinsia (revenue raised nationally shall be shared equitably among men and women of different classes, with a focus of reaching out more marginalised groups in the soceity in the country)
		  ◦ Matumizi ya mapato ya taifa yanufaishe watu wote, kwa kuzingatia mahitaji ya makundi maalum (expenditure shall promote the equitable development of the country, including by making special provision for marginalized groups and areas)
		  ◦ Matumizi ya rasilimali za taifa pamoja na mikopo itumike kwa uadilifu kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya kizazi kijacho (the benefit of the use of resources and public borrowing shall be shared equitably between the present and future generations) (v) fedha za umma zitumike kwa uadilifu na kwa njia ya uwajibikaji) Public money shall be used in a prudent and responsible way)
		  ◦ Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ufanyike kwa kufuata taratibu na misingi ya uwazi na uwajibikaji (financial management shall be responsible, and fiscal and reporting shall be clear).
		Utekelezaji wa dhana ya usawa iliyoainshwa katika ibara 202, na itakayoelezwa katika sheria zote za nchi itazingatia: (a) maslahi ya taifa (national interest (h) mahitaji ya makundi yaliyoko pembezoni (the need for affirmative action in respect of disadvantaged areas and groups).

Mtandao huu unaratibiwa na:

Women Fund Tanzania
659 Mikoroshini Street
P.O.Box 79235 Dar es Salaam
Mob: +255 753 912 130
Email: info@wft.or.tz
www.wft.or.tz